TOLEO NO: 15 MEI 07 - MEI 19 2019

TANZANIA PORTS AUTHORITY

Gazeti

www.ports.go.tz | Bendera Tatu S.L.P. 9184 Dar es Salaam | Email: ccu@ports.go.tz | Namba za Bure: 0800110032 / 0800110047

UBORESHAJI GATI 12-14 KUINGIZWA KWENYE AWAMU YA PILI YA MRADI WA DMGP

Wajumbe wa Kamati ya PIC, wakiwa katika kikao na uongozi wa Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Mamlaka.

NDANI

BANDARI YA DAR KUANZA KUHUDUMIA SHEHENA YA MZIGO WA MALAWI 05

TPA YAUPIGA JEKI MKOA WA LINDI KWENYE ELIMU NA AFYA 07

WANACHAMA BANDARINI SACOSS WASHAURIWA KUWEKEZA KATIKA MIRADI YA MAENDELEO 11

TPA KUANZISHA GATI NA ENEO MAALUMU LA KUPOKELEA MELI ZA KITALII 14

Na Focus Mauki

Mpango wa ujenzi wa Gati Namba 12-14 katika Bandari ya Dar es Salaam unatarajiwa kuingizwa kwenye Awamu ya Pili ya Mradi wa Maboresho ya Bandari unaofahamika kama Dar es Salaam Maritime Gateway Project (DMGP).

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deusdedit Kakoko ameiambia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwamba, mara baada ya kushauriana na wafadhili wa kuboresha Bandari ya Dar es Salaam, ambao ni pamoja na Benki ya Dunia, DFID na TradeMark East Africa (TMEA) imekubalika kwamba ili kuboresha bandari kwa ujumla Gati zote zikiwemo Gati Namba 12 (kwa sasa KOJ) hadi namba 15 yajumuishwe kwenye Mradi wa DMGP.

Wajumbe wa Kamati hiyo waliongozwa na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dk. Raphael Chegeni walifika katika Bandari ya Dar es Salaam hivi karibuni kwa lengo la kuona maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Ujenzi wa mradi wa DMPG Awamu ya kwanza.

Ujenzi wa gati hizo sasa umependekezwa uingie katika Awamu ya pili (phase II) mara baada ya kukamilika kwa Awamu ya kwanza ya Mradi

Wajumbe wa Kamati ya PIC, wakiwa katika kikao na uongozi wa Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Mamlaka.

Ujenzi Gati 12-14 kuingizwa kwenye awamu ya pili ya mradi wa DMGP

wa DMGP unaotarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miaka mitatu (3).

Kazi ya utekelezaji wa ujenzi wa Gati namba 1-7 pamoja na Gati mpya maalum kwa ajili ya kuhudumia Meli za magari (RoRo Berth) kwenye Bandari ya Dar es Salaam imefikia asilimia 50. Ujenzi wa Gati hiyo ya magari unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2019.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deusdedit Kakoko amesema pamoja na ujenzi wa Gati hiyo unaotarajiwa kukamilika katikati ya mwaka huu, kazi ya kuboresha Gati namba 1 imeshakamilika tangu tarehe 7 Disemba mwaka 2018.

"Mkandarasi alikamilisha kazi ya ujenzi wa Gati Namba 1 ambayo ilihusisha kuongeza eneo la kupakia na kupakua mizigo, kuongeza kina cha maji mpaka kufikia mita 14.5 na kazi kama hiyo kwenye Gati 2 mpaka 4 nayo inatarajiwa kukamilika na kukabidhiwa ifikapo mwezi Julai mwaka huu 2019," amesema Kakoko.

Mkurugenzi Mkuu amebainisha kwamba, kwa upande wa ujenzi wa Gati namba 5 mpaka 7 kwa sasa Mkandarasi anaendelea na usanifu wa kina (detailed design) ambapo ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Novemba 2019.

Mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam (DMGP) unatekelezwa kwa awamu mbili ili kutoathiri Shughuli za utekelezaji katika Bandari (port operations) wakati Mradi unaendelea.

Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mradi inahusisha maboresho ya Gati namba 1-7 pamoja na Gati jipya kwa ajili ya Meli za magari.

Gati hilo jipya linajengwa kwenye eneo la Gerezani Creek ambapo

TPA ilisaini mkataba na Mkandarasi kutoka China Kampuni ya M/s China Habour Engineering Company Limited mnamo tarehe 10 Juni 2017 kwa kipindi cha miaka mitatu huku gharama za Mradi zikikadiriwa kuwa ni zaidi ya Shilingi Bilioni 330.

Awamu ya pili ya ujenzi wa Mradi itahusisha kuongeza kina na upana wa lango la kuingilia na kugeuzia meli kitaalamu ikifahamika kama "Deepening and Widening of Entrance Channel and Turning Basin".

Mpaka sasa Mamlaka ipo katika hatua mbalimbali za maandalizi ya kutekeleza awamu hii ya pili ya Mradi ambapo zabuni ya awali (expression of interest) kwa ajili ya kupata wakandarasi wachache watakaofuzu kushindanishwa ili kumpata Mkandarasi wa kazi husika ambapo uthamini wake umekamilika na kitakachofuata ni kuwashindanisha washindi wa awali.

Hatua ya pili ya zabuni itakuwa ni "Request for Proposal-RFP" ambayo itafanyika mara baada ya kukamilika kwa tafiti na usanifu wa Mradi (Engineering Surveys, Environmental and Social Assessment and Detailed Design).

Kazi kwa ajili ya kufanya usanifu (study and design) inatarajiwa kukamilika Mei 2019 ambapo Mtaalamu Mwelekezi (Consultant M/s Technital) kutoka Italia anayeangalia namna bora ya kuongeza kina na upana wa lango la kuingilia meli na kutengeneza nyaraka (tender document) anaendelea na kazi.

Kwa upande wa kazi ya kufanya tathmini ya athari za kijamii na kimazingira (Environment and Social Impact Assessment) inafanywa na Mtaalamu Mwelekezi Kampuni ya M/s Asian Consulting Enterprise ambaye anaendelea na kazi ambapo anatarajia kuikamilisha ifikapo mwezi Mei 2019.

Mara baada ya hapo hatua ya pili baada ya tafiti na usanifu (study and design) kukamilika ni zabuni kutolewa kwa makampuni yaliyoshinda katika awamu ya kwanza (pre-qualifiification) kwa ajili ya kupata Mkandarasi wa kazi kuongeza kina na upana huo wa lango la kuingilia meli na sehemu ya kugeuzia meli kazi ambayo inatarajiwa kuanza mwezi Oktoba 2019.

Kwa kutambua ukweli kwamba usafirishaji mizigo unategemea kwa kiasi kikubwa usafiri wa wa njia ya Reli, kazi ya uboreshaji wa mtandao wa Reli ndani ya Bandari ya Dar es Salaam nayo itakuwa ni sehemu ya tatu ya maboresho katika awamu ya kwanza ya Mradi huu wa DMGP.

Kwa sasa Mtaalamu Mwelekezi (M/s Gauff) anaendelea na kazi ya usanifu (detailed design) kupitia Mradi wa "Tanzania Intermodal Transport Program-TIRP" unaosimamiwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) na kugharamiwa na Benki ya Dunia.

Kazi ya kuboresha mtandao huo wa reli inatarajiwa kuanza mara tu Mtaalamu atakapokamilisha usanifu.

Sehemu ya nne ya awamu ya kwanza ya Mradi huu pia itahusisha kuimarisha na kuongeza kina katika Gati Na. 8-11 ili ziweze kuhudumia meli kubwa na za kisasa. Katika kutekeleza sehemu ya Mradi huu TPA imeandaa hadidu za rejea (Terms

Mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam (DMGP) unatekelezwa kwa awamu mbili ili kutoathiri uendeshaji wa shughuli za Bandari (port operations) wakati wa utekelezaji wake. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mradi inahusisha maboresho ya Gati namba 1-7 pamoja na Gati jipya kwa ajili ya Meli za magari (RoRo Berth).

of Reference) kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu (feasibility study and detailed engineering design) wa Mradi.

Zabuni hii inatarajiwa kutangazwa mwezi Mei 2019 na kazi ya upembuzi yakinifu itaanza mwezi Oktoba 2019 kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza mwaka 2021 mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Gati namba 1-7.

Mara baada ya kukamilika kwa Awamu zote za Mradi wa DMGP, Bandari ya Dar es Salaam itakuwa na uwezo mkubwa wa kuhudumia meli kubwa zaidi na za kisasa. Inatarajiwa kwamba Bandari ya Dar es Salaam itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli zenye urefu (legth overall) wa mita mia tatu na tano (305) zenye uwezo wa kubeba makontena (TEUs) kati ya 7,000 mpaka 8,000.

Bandari ya Dar es Salaam pia itaongeza uwezo wa kuhudumia Shehena kubwa zaidi ya mizigo kutoka uwezo wa sasa wa kuhudumia tani milioni 16 hadi kufikia tani milioni 28 kama ilivoainishwa kwenye mpango mkakati wa Mamlaka (Corporate Strategic Plan).

Hali hii inatarajiwa pia kuongeza mapato ya TPA na Taifa kwa ujumla kutokana na uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam kuhudumia shehena kubwa zaidi.

Mpango wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam uliibuliwa kutoka katika Mpango Kabambe (Port Master Plan) wa Mamlaka wa miaka 20 (2009-2028) ambapo mwaka 2013 TPA ilikamilisha kazi ya upembuzi yakinifu wa kuboresha Gati namba 1-7.

Kazi hiyo ya upembuzi yakinifu ilihusisha kuongeza kina na kuimarisha Gati namba 1-7, kuongeza kina cha lango la kuingilia meli (entrance channel) na eneo la kugeuzia meli (turning basin) pamoja na ujenzi wa Gati jipya la kuhudumia magari (RoRo).

Katika upembuzi huo ambao uligawanyika mara mbili sehemu ya pili ilihusisha kuangalia namna bora ya kuhudumia (kupakia na kupakua shehena) shehena mbalimbali na uboreshaji wa mindombinu ndani ya Bandari ya Dar es Salaam kwa ujumla ikiwa ni pamoja na mpangilio wa Bandari (improvement of port layout).

Kazi hizo pia ni pamoja na ujenzi wa Gati mpya, barabara ziingiazo na kutoka Bandarini, reli, uhamishaji na ujenzi wa maghala, ujenzi wa maeneo ya uendeshaji (operational yards) na ufungaji wa mfumo (Conveyor Belt Systeam) wa kuhudumia shehena ya kichele (nafaka, mbolea, saruji na clinker).

Mara baada ya kazi ya upembuzi yakinifu kukamilika zilianza juhudi za kutekeleza Mradi ambapo Septemba 2014, ujumbe wa pamoja wa Wadau wa Maendeleo wakiwahusisha TradeMark East Africa, Department of International Development (DFID) na Benki ya Dunia ulifika Tanzania kwa ajili ya kuthamini Mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam na kuingia makubaliano ya awali (MoU) na Serikali ya Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi husika.

Mara baada ya MoU kusainiwa uthamini wa utekelezaji wa Mradi na shughuli mbalimbali za Mradi ziliendelea na maandalizi ya tathimini ya Mradi (project appraisal document – PAD) yalikamilika mwezi Mei 2017 ambapo makubaliano baina ya Serikali na Benki ya Dunia ya mkopo wa Dola za Marekani Milioni 345 kwa ajili ya uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam-DMGP yalisainiwa mwezi Oktoba 2017.

Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam pia utaiwezesha kuiongezea ufanisi wa utendaji na ushindani baina yake na Bandari nyingine za Ukanda wa Bahari ya Hindi kama vile Mombasa, Maputo, Beira, Nacala na Durban.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, aliwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba, TPA inatambua na kuthamini ushirikiano inaoupata kutoka Serikalini, Bunge na Kamati zake, Wadau wote wa Sekta ya uchukuzi pamoja na wahisani wa maendeleo kama vile Benki ya Dunia.

Mara baada ya kukamilika kwa awamu zote za Mradi wa DMGP Bandari ya Dar es Salaam itakuwa na uwezo mkubwa wa kuhudumia meli kubwa zaidi na za kisasa. Inatarajiwa kwamba Bandari ya Dar es Salaam itakuwa na uwezo wa kuhudumia zenye urefu (legth oberall) wa mita mia tatu na tano (305) zenye uwezo wa kubeba kontena (TEUs) kati ya 7,000 mpaka 8,000.

BANDARI YA DAR KUANZA KUHUDUMIA **SHEHENA YA MZIGO WA MALAWI KWA ASILIMIA 100**

Na Focus Mauki

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe (Mb) ameiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kujipanga kuhudumia shehena ya mzigo wa Malawi kutoka asilimia 20 hadi 100 kuanzia sasa.

Waziri Kamwelwe ametoa agizo hilo hivi karibuni wakati wa Kikao cha pamoja kati yake na Waziri wa Uchukuzi na Ujenzi wa Malawi, Mhe. Jappie Mhango (Mb) kilichofanyika jijini Dar es Salaam.

"Hivi karibuni kumetokea mvua kubwa ambazo zimesababisha uharibifu mkubwa kwenye Bandari ya Beira nchini Msumbiji pamoja na nchi ya Malawi ambayo awali ilikuwa ikiitumia Bandari hiyo kupitishia mzigo wa yake. Kutokana na uharibifu huo sasa Malawi wataitumia Bandari ya Dar es Salaam kwa asilimia 100 badala ya asilimia 20 ya awali," amefafanua Waziri Kamwelwe.

Waziri amesema kwamba Bandari ya Beira kwa sasa imeharibiwa kabisa na mafuriko yaliyotokea na jambo hilo linaifanya Malawi kuanza kutumia Bandari za Tanzania hususani Bandari ya Dar es Salaam kwa asilimia mia moja.

Pamoja na hilo, Waziri Kamwelwe amesema maamuzi ya kutumia Bandari za Tanzania pia yametokana na mazungumzo ambayo ameyafanya na Waziri mwenzake wa Malawi yaliyolenga kuimarisha mahusiano ya kibiashara baina ya nchi za Tanzania na Malawi.

Ameongeza kuwa mkutano wake na Waziri mwenzake pia umelenga kuona mahusiano baina ya nchi hizi mbili yalianza wapi na wapi wanaweza

Baadhi ya Viongozi wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Menejimenti ya TPA na Wadau wanaohusika na usafirishaji wakiwa katika kikao cha Mawaziri wa Uchukuzi wa Tanzania na Malawi.

"Hivi karibuni kumetokea mvua kubwa ambazo zimesababisha uharibifu mkubwa kwenye Bandari ya Beira nchini Msumbiji pamoja na nchi ya Malawi ambayo awali ilikuwa ikiitumia Bandari hiyo kupitishia mzigo wa Malawi, kutokana na uharibifu huo sasa Malawi wataitumia Bandari ya Dar es Salaam kwa asilimia 100 badala ya asilimia 20 ya awali,"

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe (MB) kushoto na Waziri wa Uchukuzi na Ujenzi wa Malawi, Mhe. Jappie Mhango (MB) wakiwa katika kikao hicho kilichofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

kuboresha na wamegundua kuwa tayari kulikuwa na mkataba wa mahusiano kati ya Tanzania na Malawi ambao ulisainiwa na Mawaziri wa Uchukuzi mwaka 1987.

"Bahati nzuri tumeupata na tumeupitia mkataba huo wa mahusiano ambao kimsingi ndio uliifanya Serikali ya Malawi ikajenga Bandari kavu ambayo leo inazojulikana kama Malawi Cargo hapa Dar es Salaam na Mbeya," amefafanua Waziri.

Amesema kuwa, ili kuendelea na utekelezaji wa mkataba huo, wamekubaliana kuunda timu ambayo itapitia mkataba huo ambao kimsingi haujawahi kufanyiwa marekebisho ili uweze kukidhi matakwa ya sasa ya kisheria, taratibu na kanuni kwa lengo la kuingiza mabadiliko yatakayokidhi mahitaji ya sasa ya kijamii na kibiashara.

Mhandisi Kamwelwe ameongeza kuwa, katika kutekeleza mkataba huu Mawaziri watakuwa wakikutana kila baada ya miezi sita ili kujadili mambo ya kibiashara na kwa kuanzia tayari amemuagiza Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deusdedit Kakoko kujipanga kuhudumia nyongeza ya shehena ya mzigo kutoka Malawi kwa asilimia 100.

"Ni lazima mjipange ili kuhakikisha mzigo unapita kwa haraka katika muda wanaotaka wateja wa Malawi na kwa bahati nzuri kwenye Bandari Kavu za Malawi kuna miundombinu mingi mpaka matanki ya mafuta hivyo ni matumaini yetu kwamba mzigo utaongezeka," ameongeza Waziri.

Sambamba na hilo Waziri amebainisha kwamba Serikali itahakikisha kwamba mahusiano ya kibiashara na kijamii baina ya Tanzania na Malawi yanakuwa makubwa. Ili kutekeleza hilo wamejipanga kufanya kikao kingine mwezi Juni 2019 jijini Dar es Salaam.

Inatarajiwa kwamba timu ya wataalamu mbalimbali kama vile Wanasheria, Wataalamu wa Biashara na Maafisa Mipango watapitia makubaliano ya mwaka 1987 na kuweza kuona endapo kuna haja ya kubadili kidogo baadhi ya vifungu vya makubaliano kwa lengo la kuviboresha ili kuendana na hali ya sasa.

Kwa upande wake Waziri wa Uchukuzi wa Malawi, Mhe. Mhango amesema wanaishukuru sana Serikali ya Tanzania kwa undugu mkubwa waliouonyesha kwa Wananchi wa Malawi na hasa katika kuwapatia msaada mkubwa wa madawa na chakula kwa waathirika wa mafuriko.

"Napenda kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk. John Pombe Joseph Magufuli, Waziri mwenzangu na Baraza lote la Mawaziri na wananchi wa Tanzania kwa mchango wao mkubwa kwa Serikali ya Malawi hususani kwa msaada wa chakula na madawa na tunaamini kwamba mambo mengine ya kibiashara tuliyoyajadili yatafanyiwa kazi na kupata ufumbuzi wa kudumu," amehitimisha Mhe. Mhango.

TPA YAUPIGA JEKI MKOA WA LINDI KWENYE ELIMU NA AFYA

Mkurugenzi Mkuu akikabidhi Msaada wa Mashuka na Vyandarua kwa Mkuu wa Wilaya ya Kilwa kwa ajili ya Hospitali na Vituo vya Afya Kilwa Masoko.

Na Fassie Obadia

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imetoa msaada wa madawati 76, vyandarua 541 na mashuka 500 yenye thamani ya shilingi Milioni 15 kwaa jili ya Mkoa wa Lindi hivi karibuni.

Akikabidhi msaada huo Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deusdedit Kakoko amesema, mchango huo umetolewa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Misaada kwa jamii kwa lengo la kurudisha faida inayopatikana.

"Mamlaka inatambua kwamba wakazi wa Manispaa ya Lindi na Kilwa wanatumia Bandari zetu kupitishia bidhaa zao kupeleka maeneo mbalimbali na kuingizia Mamlaka mapato, na ndio maana Mamlaka inarudisha faida yake kwa jamii," amesema Kakoko.

Akipokea Madawati hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Mhe. Shaibu Ndemanga ameipongeza TPA kwa jitihada inazofanya za kuboresha elimu Tanzania.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kilwa ameishukuru Mamlaka kwa msaada wa mashuka na vyandarua walivyotoa kwani msaada huo utasaidia kuboresha huduma hospitali na vituo vya afya kwa kuwa vilikuwa vinakabiliwa na upungufu mkubwa wa mashuka.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka Ya Usimamizi Wa Bandari Tanzania (TPA), Mhandisi Deusdedit Kakoko akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Mhe. Shaibu Ndemanga Madawati 76 kwa ajili ya Shule za Msingi Muungano, Mnazi Mmoja na Rahaleo.

"Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kilwa ameishukuru Mamlaka kwa msaada wa mashuka na vyandarua walivyotoa kwani msaada huo utasaidia kuboresha huduma hospitali na vituo vya afya kwa kuwa vilikuwa vinakabiliwa na upungufu mkubwa wa mashuka.

Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Henry Musasizi (kulia) akizungumza na Menejimenti ya Bandari ya Dar es Salaam wakati wa ziara yao hivi karibuni. Katikati ni Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Bw. Elihuruma Lema na Meneja Uhusiano na Mawasiliano, Bw. Peter Millanzi.

WAJUMBE WA KAMATI YA BUNGE WATEMBELEA **BANDARI YA DAR ES SALAAM**

Na Focus Mauki

Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Fedha, Uchumi na Mipango kutoka Bunge la Uganda wametembelea Bandari ya Dar es Salaam hivi karibuni ili kujifunza masuala ya Himaya Pamoja ya Forodha (Single Customs Territory).

Ziara ya Wabunge hao iliongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Henry Musasizi ambae alikutana na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Bw. Elihuruma Lema.

Mbali na kupatiwa maelezo kuhusiana na nafasi ya TPA kwenye Himaya ya Pamoja ya Forodha (SCT) Wakiwa katika Bandari hiyo, Wajumbe hao pia walipata fursa ya kuona maendeleo na hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa mradi wa DMGP.

Wajumbe mbalimbali wakiwa katika Kikao.

WAZIRI KAMWELWE, BODI YA TPA WABARIKI MIKAKATI YA 'DREDGING' TANGA

Aahidi kuipa baraka mikakati mbalimbali ya maboresho ya kuongeza kina cha Bandari ya sasa ili kuruhusu Meli kubwa kutia nanga gatini. Aitaka Mamlaka kuboresha Chelezo cha Bandari ya Tanga (Dockyard) kuwa Chelezo kubwa kuliko zote Afrika Mashariki

Na Moni Jarufu

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe (Mb) ameridhishwa na kuridhia mkakati wa uboreshwaji wa kuongeza kina cha Bandari ya Tanga na hivyo kuipa kibali Bodi ya Wakurugenzi ya Bandari ya TPA kuendelea na hatua mbalimbali za uboreshwaji huo ili Meli kubwa ziweze kutia nanga gatini katika Bandari ya Tanga.

Waziri pia ameiagiza Bodi ya Wakurugenzi wa TPA kuhakikisha wanajenga Chelezo "Dockyard" kubwa na ya kisasa katika Bandari ya Tanga ili ukarabati wa vyombo vyote ufanyike katika Chelezo hiyo na kupunguza gharama zinazofanyika kila mwaka nje ya Nchi.

Waziri Kamwele aliyasema hayo wakati akiwa katika ziara ya kutembelea Bandari ya Tanga hivi karibuni ili kukagua hali halisi ya sasa ya miundombinu na vifaa vya kupakua na kupakia shehena mbalimbali pamoja na utendaji kazi wa Bandari ya Tanga.

"Ndugu Mwenyekiti wa Bodi naomba mtoe kipaumbele kwa agenda hii muhimu ya kujenga Dock Yard kubwa hapa Bandari ya Tanga kwa sababu kuna nafasi kubwa ukilinganisha na ile ya Bandari ya Dar es Salaam", alisema Mhandisi Kamwelwe.

Ameongeza kwamba, kutokana na kuwepo kwa eneo katika Bandari ya Tanga anaamini nafasi ya kujenga Chelezo itakayokuwa kubwa zaidi Afrika Mashariki itapatikana na kuipunguzia Serikali gharama za ukarabati wa vyombo vya majini nje ya Nchi unaofanyika kila mwaka.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka, Mhandisi Deusdedit Kakoko alimuonyesha Waziri michoro mbalimbali ya mahitaji ya uchimbaji na uboreshaji kina wa Bandari ya Tanga ili kuziwezesha meli kubwa kutia nanga gatini, eneo litakalotumia kumwaga udongo utakaochimbwa wakati wa uongezaji kina gatini, eneo la ardhi (kandokando ya Bandari ya Tanga) linalohitajika na Bandari ya Tanga ili kuipanua Bandari ya sasa, eneo litakalojengwa gati ya kupakulia mafuta ghafi (Chongoleani Terminal) pamoja na eneo la Ras Kazone litakalojengwa gati ya kupakulia mafuta.

Kwa upande wake Meneja Bandari ya Tanga, Bwana Percival Salama amemueleza Waziri kuwa kwa sasa Bandari ya Tanga inahudumia meli zikiwa nangani kutokana na kuwa na gati zenye kina kifupi cha bahari hivyo kusababisha mzigo mmoja kuhudumiwa mara mbili (nangani na gatini) jambo ambalo linasababisha ongezeko la gharama za uhudumiaji mzigo huo kwa Bandari yetu.

> *Ameongeza kuwa kutokana na kuona ukubwa wa Bandari ya Tanga anaamini nafasi ya kujenga Chelezo itakayokuwa kubwa zaidi Afrika Mashariki itapatikana na kuipunguzia Serikali gharama za ukarabati wa vyombo vya majini nje ya Nchi unaofanyika kila mwaka.*

Akielezea Shehena inayohudumiwa katika Bandari ya Tanga, Bw. Salama amesema kuwa kwa sasa Bandari ya Tanga inahudumia bidhaa nyingi za mashambani ikiwemo shehena ya mkonge, mbao, macadamia na bidhaa nyingine nyingi.

Ziara ya Waziri katika Bandari ya Tanga imempa uelewa wa mahitaji halisi ya uboreshaji wa kuongeza kina cha bandari ya sasa ili kuruhusu meli kubwa ziweze kutia nanga gatini bandarini hapo.

Akiwa katika ziara hiyo Waziri aliongozana na Bodi ya Wakurugenzi ya TPA na kukagua ukarabati wa gati namba mbili, eneo la Chelezo, eneo la midaki (Scanner) pamoja na kutembelea Gati la meli za mafuta lililopo katika eneo la Ras Kazone Jijini Tanga.

Ziara yake inategemewa kuwa na Matokeo chanya ya kuboresha Bandari ya Tanga na kuwa moja ya Bandari Bora na inayovutia wateja katika Ukanda wa Afrika Mashariki.

Mwenyekiti Wa Bodi Ya Tpa Prof. Ignas Rubaratuka Akikabidhi Mabati 1,852 Kwa Mkuu Wa Wilaya Ya Mtwara Mh. Evod Mmanda Aliyemuwakilisha Mkuu Wa Mkoa Wa Mtwara

TPA YACHANGIA MABATI 1,852
KUKAMILISHA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 48

Na Fassie Obadia

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imechangia mabati 1,852 kusaidia ujenzi wa madarasa 37 katika shule 15 za Mkoa wa Mtwara.

Mchango huo wa TPA unatarajiwa kuwa faraja kwa Mkoa wa Mtwara na kuweka mazingira mazuri ya kusomea hasa kwa kuwanusuru baadhi ya Wanafunzi ambao walikuwa wanasomea chini ya miti.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Mtwara aliiomba TPA kusaidia ikiwa kama mdau mkubwa wa maendeleo ya Mkoa kukabiliana na changamoto hiyo ya kuchangia vifaa mbalimbali vya kujengea vyumba 48 vya Madarasa.

Hatimaye azma hiyo sasa imefanikiwa kupitia mchango uliotolewa wa bati 1,852 zenye thamani ya shilingi milioni 50 pamoja na madawati sabini na sita (76) yenye thamani ya shilingi milioni 15.

Akiongea wakati wa kukabidhi msaada huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TPA, Prof. Ignas Rubaratuka amesema TPA inaunga mkono jitihada zinazofanywa na Serikali za kuboresha elimu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deusdedit Kakoko amesema, "Mamlaka inatambua umuhimu wa kushiriki katika kuchangia jamii ili kuinua ustawi wa jamii katika sekta za elimu na afya."

Akipokea Msaada huo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa Mtwara, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Mhe. Evodius Mmanda aliishukuru Mamlaka kwa kutoa Msaada huo na kwa kuunga mkono jitihada za Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Pombe Joseph Magufuli za kuinua sekta ya elimu Tanzania.

Mmanda amewaasa wazazi wa kijiji cha Mwenge kuhakikisha kwamba, watoto wanasoma na jitihada zifanyike kuendelea kujenga madarasa mengine katika maeneo yao ili kufanikisha jitihada za Serikali na kuishukuru TPA kwa kujitoa kwao katika kuchangia masuala mbalimbali ya kijamii.

Mmanda amewaasa wazazi wa kijiji cha Mwenge kuhakikisha kwamba watoto wanasoma na jitihada zifanyike kuendelea kujenga madarasa mengine katika maeneo yao ili kufanikisha jitihada za Serikali na kuishukuru TPA kwa kujitoa kwao katika kuchangia masuala mbalimbali ya kijamii.

WANACHAMA BANDARINI SACOSS WASHAURIWA KUWEKEZA KATIKA MIRADI YA MAENDELEO

Na Innocent Mhando

Wanachama chama cha Akiba na Mikopo Bandarini SACCOS wameshauriwa kutumia fursa ya mikopo ili kuwekeza katika miradi ya maendeleo kwa lengo la kujikwamua kiuchumi.

Ushauri huo umetolewa na Mgeni Rasmi Meneja Bandari Msaidizi (Utekelezaji), Bw. Ahmed Mchalaganya alipokuwa anaongea na Wanachama mara baada ya kutembelea mradi wa Mabwawa ya Samaki Kigamboni.

Amesema Wanachama hawana budi kuachana na tabia ya kuchukua mikopo na kuponda starehe badala yake wawekeze katika miradi ya maendeleo ili kujikwamua kiuchumi.

"Sikujua kama nakuja kujionea mradi mkubwa kama huu kwa kweli mnastahili pongezi nyingi, ila niwahusie wengine waachane na hulka ya kuchukua mikopo na kuitumia kuponda starehe badala ya kuwekeza katika miradi ya maendeleo." Alisema Mchalaganya.

Amesema kuwa, miradi hiyo ya mendeleo sio tu kuwasaidia Wanachama kujikwamua kiuchumi na kujiongezea kipato pia itawawezesha kuishi vizuri hata baada ya kustaafu.

"tuwekeze katika miradi ya maendeleo kwa kuwa ipo siku itatusaidia na kuepekuna na mishituko ya maisha ambayo kwa namna moja au ingine inapelekea kupata magonjwa nyemelezi" Alisisitiza Mchalaganya.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi DOWUTA Bw. Mashaka Karume wakati akitoa nasaha zake amewataka wanachama kuwekeza wakiwa bado na nguvu za ujana pasipo kusubiri mpaka umri mkubwa ndiyo waanze kuwekeza.

"zamani nilikuwa nadhani muda wa kuwekeza ni mpaka uwe na umri mkubwa kumbe nilikuwa nakosea , wakati wa kuwekeza ni sasa tukiwa na nguvu , tusisubiri mpaka tukiwa tumechoka ndipo tuwekeze, yatupasa kuwekeza tukiwa vijana ili kufaidi matunda ya uwekezji huku tukiwa na nguvu" . Alisema Karume.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama cha Akiba na Mikopo Bandarini Saccos, Bi Stella Mutayabarwa amesema kuwa, madhumuni ya mradi huo ni kuwewezesha wanachama wake kujiongezea kipato na pia chama kukuza mtaji wake.

"Tumeuanzisha mradi huu kwa lengo la kuboresha kipato cha Wanachama wetu kwa kuwawezesha kukodisha mabwawa hayo na kuanzisha ufuguaji wa samaki, mradi ambao naamini utawaongezea kipato wanachama wetu na pia kukiogezea chama faida," alisema Mutayabarwa.

Aidha aliwataka Wanachama wanapochukua mikopo wawe wameshajiwekea malengo ya namna ya kujianzishia miradi mbalimbali kuliko hali ilivyo sasa wengi wao wanakopa huku hawana malengo maalum.

Mabwawa hayo 6 yapo tayari kwa kuanza ufugaji huku mengine mawili yapo katika ujenzi ambapo yatakuwa na uwezo wa kufugia kati ya samaki 15,000 hadi 20,000.

"Ndoto na Mafanikio zinaanzia kwenye SACCOS".

Baadhi wa Wanachama wa SACCOS wakiwa katika picha ya pamoja.

Wajumbe wa Mkutano wakiwa katika picha ya pamoja.

BANDARI YA TANGA YAWAHAKIKISHIA HUDUMA BORA

WATEJA NA WAFANYABIASHARA WA MIKOA YA ARUSHA NA KILIMANJARO

Na Moni Jarufu

Wateja wa Bandari ya Tanga wa Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha wamefanya ziara ya kutembelea Bandari ya Tanga hivi karibuni na kujionea shughuli za kupakia na kupakua shehena mbalimbali pamoja na kujionea maboresho yaliyofanyika bandarini hapo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TPA, wakati wa mkutano na Wateja hao uliofanyika katika ukumbi wa mkutano katika jengo la "Bandari House" Kaimu Meneja Masoko wa TPA, Bi. Lydia Mallya amesema kuwa lengo la TPA kualika Wateja kutembelea Bandari ya Tanga ni kujionea wenyewe uboreshaji wa huduma uliofanywa na TPA katika miaka ya hivi karibuni.

Uboreshaji huo unaifanya Bandari ya Tanga kuwa moja ya bandari zinazotoa huduma kwa kasi zaidi hivyo kumpunguzia Mteja gharama ya kufanya biashara.

Bi. Lydia aliwashukuru Wateja hao kwa kukubali mwaliko na kutekeleza kwa vitendo kutembelea Bandari ya Tanga.

> *mikakati kadhaa waliyoiweka kuirudisha Bandari ya Tanga kwenye hadhi yake alisema ni kuchimba kuongeza kina eneo la gatini ili kuwezesha meli kubwa kutia nanga gatini.*

Aliwaomba wateja hao kuitumia bandari hiyo ili kufaidika na ukaribu na ubora wa huduma katika Bandari ya Tanga.

Kwa upande wake Meneja wa Bandari ya Tanga, Bw. Percival Salama amewahakikishia Wateja hao kuwa Bandari ya Tanga kwa sasa hakuna urasimu unaokwamisha ufanyaji wa biashara na Taasisi zote zinazotoa huduma katika bandari zina ushirikiano wa hali ya juu saa 24 hivyo waondoe wasiwasi wa kutumia Bandari hiyo ya Tanga.

Bw. Salama aliweka wazi mikakati kadhaa waliyoiweka kuirudisha Bandari ya Tanga kwenye hadhi yake ambapo alisema "kuchimba kuongeza kina eneo la gatini ili kuwezesha meli kubwa kutia nanga gatini, kuwepo na kutekeleza mkataba wa huduma kwa Mteja, kuwepo kwa vikao vya kila mwezi na wadau wote wa Bandari vinavyolenga kuboresha utoaji huduma.

Mikakati mingine ni pamoja na kuwepo kwa mitambo ya kutosha ya upakuaji na upakiaji wa shehena, ununuzi wa mitambo mipya 20 katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo mitambo 9 tayari imekwisha pokelewa pamoja na kuwepo kwa ushirikiano mkubwa kati ya TPA na Taasisi zenye wajibu wa kisheria Bandarini kama TRA, TBS, GCLA, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na TFDA kunarahisisha utoaji huduma na hivyo kuondokana na urasimu unaosemwa kuwepo miaka ya nyuma."

Awali Mwenyekiti aliyeongoza kikao cha Wateja hao, Bw. Bwai Biseko (Katibu Tawala Msaidizi-Utawala Mkoa wa Kilimanjaro) wakati akifungua na baadaye kuongoza majadiliano katika kikao hicho alisema pamoja na mambo mengine umuhimu wa TPA kuzingatia makubaliano yaliyopo kwenye mkataba wa Huduma kwa Mteja (Customer Service Charter) ili kuimarisha utoaji wa huduma na hivyo kuaminika kwa Wateja wanaotumia Bandari ya Tanga.

Aliwataka Wateja waliopata fursa ya kutembelea Bandari ya Tanga, kuwa mabalozi wa mambo mema na mazuri na kuimarika kwa ubora wa huduma zinazotolewa na Bandari ya Tanga ambazo zimethibitishwa na baadhi ya Wateja kama TPPL na mawakala wa forodha ni uthibitisho tosha wa mabadiliko makubwa ya kiutendaji na utoaji wa Huduma katika Bandari ya Tanga.

Aliwataka wale ambao hawajaanza kupitisha shehena zao katika Bandari ya Tanga kutokana na changamoto za kiutendaji za miaka ya nyuma sasa waanze maana huduma zimeboreshwa sana.

Ziara ya wadau hao katika Bandari ya Tanga ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Kakoko wakati alipofanya mkutano na Wafanyabiashara hao katika Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha hivi karibuni na aliwataka waje kujionea wenyewe utendaji wa Bandari ya Tanga na maboresho mbalimbali yaliyofanyika katika Bandari hiyo.

TPA YAKUTANANISHA WADAU KUJADILI MAPENDEKEZO YA KUBORESHA SHERIA YA BANDARI!

Na Focus Mauki

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imewakutanisha Wadau wake mbalimbali kwa lengo la kujadili mapendekezo mbalimbali ya kuboresha sheria ya Bandari na 17 ya mwaka 2004.

Akizungumza wakati wa kufungua kikao hicho kilichofanyika kwenye ofisi za TPA Makao Makuu, Mwenyekiti wa kikao hicho, Eng. Kisaka ambaye ni Mkurugenzi katika Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano amesema kwamba lengo la kikao hicho ni kupitia mapendekezo yaloyowasilishwa na TPA katika kurejea sheria hiyo ambayo haijawahi kufanyiwa marekebisho kwa kipindi kirefu ili kukidhi hitaji la sasa la uendeshaji wa shughuli za Bandari.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria TPA, Bi. Leticia Mtaki amesema baadhi ya maboresho yaliyopendekezwa ni pamoja na kudhibiti bandari bubu na kuongeza wigo wa utendaji wa bandari.

Hatua itakayofuata mara baada ya mapendekezo ya kikao hicho ni kuingiza maoni hayo ya wadau katika rasimu inayoprndekezwa na kuiwasilisha tena kwa wadau kabla haijawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Meli ya kitalii ikiwa katika Bandari ya Dar es Salaam hivi karibu.

TPA KUANZISHA GATI NA ENEO MAALUMU LA KUPOKELEA MELI ZA KITALII

Na Focus Mauki

Meneja wa Bandari ya Dar es Salaam, Bw. Freddy Liundi amesema TPA ipo mbioni kuanzisha gati maalumu ambayo itakuwa na uwezo wa kupokea meli za kitalii (cruise ships)

Liundi amesema hayo wakati wa hafla fupi ya kupokea meli ya kitalii iliyotia nanga ndani ya Bandari ya Dar es Salaam ikiwa na watalii zaidi ya mia nne (400), ambapo takribani watalii mia moja hamsini (150) walienda kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii kabla ya kuelekea Zanzibar.

Amebainisha kwamba kwenye mipango ya muda mrefu Mamlaka ina mpango wa kujenga gati maalumu kabisa kwa watalii ambapo kutakuwa na huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na sehemu ya mapokezi kwa ajili ya maafisa wa uhamiaji, vyombo vya fedha pamoja na taasisi nyingine zote zinazohusika na mapokezi ya meli za kitalii.

"Mamlaka ina mipango ya muda mrefu na muda mfupi ili kuhakikisha tunakuwa na uwezo wa kupokelea meli za watalii katika eneo na gati maalumu ya kupokelea meli za aina hiyo," ameongeza Liundi.

Liundi ameongeza kwamba kwa sasa Mamlaka inaendelea kukamilisha ujenzi wa gati mpya ambayo kimsingi ni kwa ajili ya kushushia magari (RoRo). Gati hiyo pia itatumika kwa huduma mbalimbali (multipurpose) ikiwa ni pamoja na kupokea meli za kitalii.

Ameongeza kwamba Meli hiyo ya kitalii ambayo imetia nanga katika bandari hiyo ina takribani urefu wa mita mia moja na sabini (170) lakini gati ambayo inajengwa itakuwa na uwezo wa kupokea meli yenye urefu wa zaidi ya mita 300.

"Duniani kuna meli kubwa na ndefu za kitalii, kitu muhimu gati ambayo tunaenda kuikamilisha itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli ya mita 350. Meli ya urefu huo ni kubwa sana kwani ina uwezo wa kubeba watalii elfu nne mpaka elfu tano kwa wakati mmoja. Katika mipango ya muda mfupi kuanzia mwezi Septemba mwaka huu tutakuwa na uwezo wa kupokea meli zenye ukubwa huo," amefafanua Liundi.

Sambamba na hilo Liundi ameongeza kwamba, TPA pia itazingatia ukweli kwamba meli nyingi za kitalii zinakuja na wazee na watu wenye ulemavu hivyo gati hilo jipya litakuwa na miundombinu maalum ya kuweza kuwapokea watalii wenye hali hiyo katika kiwango cha kimataifa.

Awali, akizungumzia ujio wa Meli hiyo ya Kitalii, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Alois Nzuki amesema biashara ya utalii wa meli zina manufaa makubwa sana kwa nchi kwani kwa sasa duniani kuna meli zinazobeba abiria 4000 mpaka 5000.

Ameongeza kuwa, Tanzania ina bahati moja kubwa kwa sababu waandaji wa meli za kitalii wanafahamu vizuri sana Tanzania kwamba, ukifika Tanzania unaweza kutembelea jiji lenyewe la Dar es Salaam kwa maana ya maeneo ya kihistoria pamoja na vivutio vingine vya karibu kama vile mbuga ya wanyama mikumi, Zanzibar, Serengeti na mbuga ya Selous.

Pamoja na bahati hiyo ya kuwa na vivutio hivyo waandaji hao wa ratiba ya meli za kitalii, wameiomba Tanzania hususani

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kujenga gati na eneo mahsusi ambalo litakuwa likitumika kwa ajili ya kupokea meli za kitalii kubwa zaidi na hivyo kuiongozea Serikali mapato.

Dk. Nzuki amesema kuna kila sababu ya kutenga gati na eneo mahususi lenye huduma zote za uhamiaji, forodha na mabenki ili kuhudumia watalii na itapendeza likiwa ni jengo moja na amemshukuru Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deusdedit Kakoko kwa kuanza kulifanyia kazi wazo hilo.

"Ninashukuru sana Mamlaka ya Bandari wametuelewa, Mkurugenzi Mkuu, Eng. Kakoko amenielewa na tunakwenda vizuri kwamba katika upanuzi wa Bandari ambao unaoendelea patakuwa na gati na jengo mahsusi kwa ajili ya kupokea watalii wanaokuja kwa meli," ameongeza Dk. Nzuki.

Ameongeza kuwa waandaji wa meli wameidhibitishia Serikali kwamba, endapo kutakuwa na gati na jengo mahsusi wataweza kuipanga Tanzania kwenye ratiba ya meli za kuja Bandari ya Dar es Salaam kila wiki na kutakuwa na meli kwa wastani mbili mpaka tatu kwa wiki.

Faida za kupokea meli za kitalii ni kubwa kwa uchumi wa nchi na ni muhimu kuwekeza kwenye utalii wa meli kwani watalii wanaoshuka na kwenye maeneo mbalimbali wanatumia pesa na wananchi wa wanaouza vifaa vya utalii, maduka ya fedha za kigeni na vyombo vya usafiri watapata pesa na faida kuwa kubwa kwenye uchumi wa jumla mbali na TPA kupata faida pekee.

Amesema katika mkakati wa kupanua wigo wa sekta ya utalii kama ambavyo imeagizwa na Serikali kupitia ilani ya Chama cha Mapinduzi ni muhimu kwa wadau wote wakashirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kukuza uchumi wa nchi.

Duniani kwa sasa kuna meli takribani themanini (80) ambazo zinajengwa, hivyo sekta hii inakuwa na ni muhimu kwa Serikali kuu pamoja na wadau wote kushirikiana ili kuhakikisha kwamba fursa na soko ililopo linatumika ipasavyo na tunachohitaji tu ni kuwa na hilo gati na jengo mahsusi kwa ajili ya kupokelea watalii.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mwendeshaji wa Bodi ya Utalii Tanzania, Devota Mdachi amesema watalii waliokuja na meli hiyo inayofahamika kama Silver Whispers wanatarajiwa kutembelea sehemu mbalimbali za vivutio mfano kituo cha tingatinga kilichopo Osterbay, Makumbusho ya Taifa na kisiwa cha Zanzibar.

Ameongeza kwamba ujio wa meli kubwa za kitalii nchini ni kiashiria kwamba, Tanzania ni nchi salama yenye kuvutia na wenye meli kubwa za kitalii wataendelea kuhamasika kuleta meli kubwa zaidi za kitalii nchini.

"Ujio wa meli hizi kubwa ni kiashiria kwamba, Tanzania ni nchi salama kama unavyofahamu kuna nchi ambazo zina fukwe lakini meli za kitalii kubwa na namna hii haziwezi kutumia fukwe hizo kwa sababu ya suala la usalama, pia inawapa hamasa wenye meli kubwa za kitalii kama hizi kuleta watalii wengi zaidi kuja kutembelea Tanzania," ameongeza Mdachi.

Pamoja na hilo, ametoa wito kwa wawekezaji kuchangamkia fursa kwani zipo fursa nyingi katika utalii wa fukwe, ambapo meli kubwa kama hizi zinahitaji huduma mbalimbali ambazo watalii watazihitaji kwenye kituo cha kupokea wageni, mawakala nao wana fursa ya kuwapokea na wajasirimali wadogowado wa Dar es Salaam nao wana fursa za kuuza bidhaa mbalimbali kwa watalii.

TPA YAKABIDHI MABATI 379 KWA SHULE YA SEKONDARI TANGA UFUNDI

Na Moni Jarufu

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imekabidhi jumla ya mabati 379 yenye thamani ya shilingi milioni 15 kwa shule ya Sekondari ya Tanga ufundi kwa ajili ya kuezekea nyumba 5 za walimu ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano ya Rais Dk. John Pombe Joseph Magufuli za upatikanaji wa elimu bora nchini.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mabati hayo kwa uongozi wa Shule hiyo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, Prof. Ignas Rubaratuka amesema kuwa wao kama TPA wameona ni vyema warudishe kwa jamii kile wanachokipata katika kuchangia nyanja mbalimbali kama vile elimu, afya na maendeleo ya jamii.

"Ili kuwa na Elimu bora ni lazima kuwe na mazingira bora ya ufundishaji pamoja na mambo mengine muhimu yanayotakiwa katika elimu hivyo wameona ni vyema wachangie katika kuboresha mazingira ya walimu kwani Walimu ni sehemu muhimu katika kutoa elimu bora," amesema Prof. Rubaratuka.

Ameongeza kuwa, "kwa shule hii leo tunatatoa mabati haya 379 yatakayosaidia kupaua nyumba 5 za Walimu na tunaamini kuwa yatasaidia kuboresha mazingira ya walimu ambao watatoa elimu bora kwa wanafunzi wetu ambao ndio tegemeo la Taifa na tunatarajia watakuwa Wafanyakazi wetu wa Bandari baadaye."

Akipokea msaada huo kwa niaba ya Uongozi wa shule hiyo Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Mhe. Thobias Mwilapwa ameishukuru TPA kwa kutoa msaada huo ambao amesema utapunguza upungufu wa nyumba za walimu pamoja na bwalo la Chakula la Wanafunzi katika shule hiyo.

Mhe. Mwilapwa ameoiomba TPA kuendelea kutoa misaada shuleni hapo kwa kuwa inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo miundombinu mibovu ya mfumo wa maji taka pamoja na ujenzi wa uzio wa shule.

Awali akimkaribisha Mwenyekiti wa Bodi ya TPA, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka, Mhandisi Deusdedit Kakoko amesema kuwa TPA imekuwa ikitenga bajeti maalum kila mwaka kwa ajili ya kuchangia shughuli mbalimbali katika Jamii (CSR) nchi nzima na kwa mwaka huu wa Fedha iliyotengwa na TPA ni takribani shilingi milioni 50 kwa ajili ya kuchangia mahitaji mbalimbali katika Wilaya zilizoko Mkoani Tanga.

Mhandisi Kakoko ameendelea kwa kusema kuwa, kwenye mapato wanaamini Bandari ndio Taasisi pekee kati ya Taasisi zote za umma na binafsi zinazotoa mchango mkubwa kwenye Serikali, hivyo TPA ikishapata mapato hayo inahakikisha kuwakumbuka kwa kuchangia kiasi cha faida inayopata kwa kutatua changamoto mbalimbali za jamii wanaozungukwa na Mamlaka ya Bandari .

Naye Mkuu wa Shule hiyo, Bw. Andrew Mwakanyamale ameishukuru TPA kwa msaada waliopatiwa na kusema kuwa, msaada huo utasaidia kukarabati maeneo mbalimbali ya shule hiyo na hatimaye kuboresha maendeleo ya elimu shuleni hapo na kuongeza ufaulu wa shule hiyo.

TPA imekuwa ikitenga bajeti maalum kila mwaka kwa ajili ya kuchangia shughuli mbalimbali katika Jamii (CSR) nchi nzima na kwa mwaka huu wa Fedha iliyotengwa na TPA ni takribani shilingi milioni 50 kwa ajili ya kuchangia mahitaji mbalimbali katika Wilaya zilizoko Mkoani Tanga.

Wakurugenzi wa Bodi na Menejimenti ya TPA wakikabidhi msaada wa mabati kwa Uongozi wa Wilaya.